TAARIFA HALISI NAMBA MOJA

KWA NINI TUONGEZE KASI YA KUZUIA MAAMBUKIZI YA VVU?

Mpango madhubuti na kamilifu, wa kuzuia maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI unaweza kupunguza kiasi cha millioni 29, au asilimia sitini na tatu (63%) ya maambukizi mapya 45 milioni yanayokadiriwa kutokea duniani kote kati ya mwaka 2002 na 2010; yaani yakawa milioni 16 tu.

Pamoja na jitihada za kitaifa na kimataifa za kupambana na ugonjwa wa UKIMWI, kiwango cha maambukizi mapya kiliendelea kupanda mwaka 2005 katika nchi nyingi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara eneo ambalo ndilo limeathirika zaidi duniani.

Katika maambukizi mapya milioni tano yaliyoorodheshwa duniani mwaka 2005, milioni 3.2 (asilimia 64) ni kutoka Afrika, kusini mwa Jangwa la Sahara.

Nchini Tanzania, maambukizi mapya katika mwaka wa 2005 yalikadiriwa kuwa chini ya laki 2 (yaani watu 197,195), kati ya haya maambukizi mijini yalikuwa 74,925 na vijijini 122 270

Ugonjwa wa UKIMWI ndio tishio kubwa zaidi kwa usalama na maendeleo ya Afrika ambapo husababisha malengo mengi ya kimaendeleo ambayo yamekubaliwa kimataifa kushindwa kutekelezeka. Bila kuongeza kasi ya kuzuia maambukizi, UKIMWI utaendelea kurudisha nyuma maendeleo yaliyopatikana na kuongeza umaskini na mateso kwa binadamu barani Afrika.

Kila mmoja wetu anafahamu jinsi Tanzania tulivyo nyuma kimaendeleo na tukiongeza na mlipuko wa ugonjwa wa UKIMWI ni vigumu sana kukamilisha shughuli nyingi za maendeleo hapa nchini.
Mahitaji yanayoongezeka ya huduma na tiba yatazidi rasilimali chache zilizopo. Watoto wengi zaidi watabaki yatima huku kipato kidogo cha familia na jamii kikitumika kuwapa huduma na tiba. Mamilioni zaidi ya watu wataendelea kuambukizwa na kufa.

- Tangu mwaka 1980 watu milioni 50 wameambukizwa barani Afrika, ambapo milioni 22 miongoni mwao wamekwisha kufa, wengi wao katika umri muhimu kwa nguvu kazi ya taifa. *Nchini Nigeria asilimia 20 ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI hivi sasa ni watumishi wa umma. Zambia inaweza kupoteza asilimia 20 ya nguvu kazi yake ifikapo mwaka 2020 ambapo Msumbiji inaweza kupoteza waalimu wapatao 19,000 kutokana na UKIMWI kati ya mwaka 2000 na 2010.*

TAARIFA HALISI NAMBA MOJA

Hapa Tanzania hadi sasa watu wapatao 192,532 wameripotiwa kuwa wameugua ugonjwa wa UKIMWI tangu 1983 hadi 2005, kati ya watu karibu milioni mbili wanaoishi na VVU.

- Vifo vya watoto, ambavyo vilikuwa vimepungua kwa karibu nusu kati ya mwaka 1960 na 1990, vimeanza tena kuongezeka katika nchi nyingi kutokana na maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI na ukosefu wa matunzo kutokana na wazazi wengi kufariki kwa ugonjwa wa UKIMWI. Kutokana na utafiti uliofanyika nchini Malawi, mtoto ambaye mama yake amefariki ana uwezekano wa mara tatu zaidi wa kufariki kuliko mtoto ambaye mama yake yuko.

Hakuna tofauti kubwa katika nchi nyingine katika maeneo ya ukanda huu ikiwemo Tanzania.

- Kiwango cha umri wa kuishi kimepungua kwa zaidi ya miaka 15 katika nchi tano barani Afrika, ambapo katika nchi nyingine tisa kiwango hicho kimeshuka kwa kati ya miaka sita hadi 15. Mtoto anayezaliwa nchini Zambia leo anatarajia kuishi kwa miaka 32 tu ambapo nchini Afrika Kusini kiwango cha juu cha kuishi kimeshuka kutoka miaka 61 hadi miaka 51.

Nchini Tanzania kiwango hicho kimeshuka kutoka zaidi ya miaka 56 na kufikia miaka 47 hivi sasa.

- Pato la jumla (GDP) hushuka kwa kiwango cha asilimia moja kwa mwaka katika nchi ambayo kiwango cha maambukizi kimefikia asilimia nane (8%).

Tanzania hivi sasa tuko asilimia saba (7%) kutoka kiwango cha zaidi ya 10 miaka kadhaa iliyopita.

- UKIMWI umesababisha bara la Afrika lishindwe kujitosheleza kwa chakula, watoto na wazee wameachwa peke yao katika shughuli za kilimo. *Kwa mfano, inakadiriwa kuwa uzalishaji wa kilimo nchini Kenya unakadiriwa kupungua kwa asilimia 2.4 ifikapo mwaka 2010.* Usalama wa chakula barani humu uko mashakani kutokana na athari za UKIMWI katika kilimo.

- Zaidi ya watoto milioni 12 wa kiafrika wameachwa yatima na kukosa upendo, huduma na ulinzi ambao kwa kawaida hutoka kwa wazazi, wengi wa watoto hao wako mitaani. **Nchini Tanzania kuna watoto yatima karibu milioni mbili.**

TAARIFA HALISI NAMBA MOJA

Elimu ni Nguvu ya Kinga dhidi ya UKIMWI

- Kila mmoja wetu anahitaji taarifa za uhakika kuhusu Virusi Vya UKIMWI na UKIMWI. Hatua muhimu katika kuhakikisha kuwa mkakati wa kuongeza kasi ya kuzuia maambukizi unafanikiwa ni kupata elimu na taarifa nyingi iwezekanavyo, kuhusu mwelekeo wa sasa wa UKIMWI barani Afrika na mambo yanayosababisha maambukizi hayo. **Hapa nchini mkazo mkubwa unawekwa katika kuelimisha rika zote na hasa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kupata maambukizi wakiwemo vijana wa mashuleni na nje ya shule.**

- Wanawake na watoto hivi sasa wanawakilisha asilimia 60 ya watu wote walioambukizwa Virusi Vya UKIMWI barani Afrika na karibu nusu ya maambukizi mapya hutokea kwa watoto na vijana wa kati ya miaka kati ya 15 hadi 24. **Hapa Tanzania asilimia 55 ya maambukizi yote ya virusi vya UKIMWI ni wanawake, kadhalika vijana umri wa miaka 15-24 ndiyo wanaoathirika zaidi.**

- Wanawake, hasa vijana wanaathirika zaidi kisaikolojia kuhusu kuambukizwa na pia wanawake wana uwezekano wa kuambukizwa mara mbili ya wanaume wakati wanapokuwa katika kufanya mapenzi. **Hali hii ni karibu sawa katika nchi zote Kusini mwa Jangwa la Sahara**

- Huduma za afya katika bara hili kwa ujumla ni duni. Kadhalika, upo upungufu mkubwa wa vifaa vinavyohitajika katika kutibu magonjwa ya ngono ambapo kwa kawaida kuongezeka kwa maambukizi ya magonjwa ya ngono huongeza uwezekano wa maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI **kwa asilimia karibu arobaini.**

- Ukosefu wa huduma za ushauri nasaha hasa kwa vijana ni kizuizi cha kinga. Vijana wengi hasa wasichana, bado hawana taarifa juu ya namna ya kujikinga wasiambukizwe VVU.

- Masuala ya kimila na jinsia yanapaswa kuzungumzwa, ikiwa ni pamoja na mila potofu zinazokandamiza wanawake, ndoa za utotoni na ngono ya wapenzi wengi. Kujihusisha kimapenzi na wapenzi wengi kwa kipindi kimoja ni kipengele muhimu katika maambukizi ya VVU, kwa sababu kuna uwezekano wa maambukizi mara 10 hadi 100 kwa kuambukiza wengine katika mwezi wa kwanza ambao mtu hupata maambukizi.

- Kutokuwepo usawa wa kijinsia huwafanya wasichana washindwe kukataa ngono hatarishi, hivyo kuwaweka kwenye uwezekano mkubwa wa kupata maambukizi. Mila potofu na unyeti unaozingira suala zima la kujamiiana zinapaswa kupigwa vita ili upashanaji taarifa

uweze kuwa mkubwa na ufanyike kwa uwazi zaidi.

- Wanawake wanapaswa kushirikishwa katika kuhakikisha usawa wa kijinsia unakuwepo, na kubadilisha tabia za vijana wa kiume zinazoweka wasichana kwenye hatari zaidi ya kuambukizwa.

- Masuala ya kiuchumi kama vile ukame, utandawazi, ukosefu wa ajira na umaskini uliokithiri, huwafanya wanawake na vijana kujiingiza zaidi kwenye ngono isiyo salama.

Nini kifanyike

Lengo la dunia kwa ajili ya Kinga, huduma na Tiba ya UKIMWI ifikapo mwaka 2010 litafikiwa tu endapo masuala yahusuyo kinga yatafanikiwa. Kuharakisha kinga kunahitaji mambo yafuatayo:-

- Kuelekeza nguvu kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi kama vile wanawake na vijana walio katika mazingira magumu, au wanaofanya biashara ya ngono.
- Kuainisha mikakati kwa kila nchi na kuiendeleza ili iweze kuleta mafanikio.
- Kuboresha huduma za Afya zilizopo
- Kuongeza rasilimali zilizopo kwa ajili ya shughuli za kinga.